

COWS ON MILK STRIKE

[Sauti za ng'ombe zinasikika]

Mwiza: Masanja, umekamua lita ngapi leo? Oda ya maziwa imeongezeka, na Zebi anasubiria.

Masanja: Ng'ombe wamegoma, nimekamua lita kumi tu.

Mwiza: [Harshly] Nini! Nataka kuwaona hao ng'ombe waliogoma leo. Sikutegemea wanifanyie hivyo.

Zebi: Mwiza, nitachanganya nini kwenye uji wa mwanangu?!

Mwiza: Aah! Zebi, kwani maziwa ni kwa ajili ya mtoto? Nilifikiri ni ya kwako.

Zebi: Nimeshauriwa kliniki kuanza kulisha watoto chakula chenye virutubisho kuanzia umri wa miezi sita. Mwanangu ana miezi saba.

Mwiza: Mbona vyakula vyenye virutubisho ni vingi?

Zebi: Kweli, kama vipi?

Mwiza: Pika dagaa kidogo au mchicha au viazi vitamu pondaponda umlishe. Uji wake changanya na karanga zilizosagwa umlishe.

Zebi: Hivi vyakula si gharama, na vinapatikana hapa kijijini.

Mwiza: Ndiyo, pia endelea kumnyonyesha.

Zebi: Umenifumbua macho, ngoja nikampikie mwanangu viazi na dagaa. Sihitaji kununua maziwa.

Anapotimiza miezi sita, mtoto anapaswa kulishwa pia vyakula vya aina mbalimbali kama samaki, kuku, jamii ya kunde, dagaa, karanga, mbogamboga, matunda na nyama iliyopondwa, ili kumwezesha kupata virutubishi vya kutosha.